ST.MAXIMILLIANCOLBE COLLEGE
P.O.Box 905 Tabora Tel: +255 755 550 335
Email: stmaximilliancolbe@gmail.com
Website: www.stmaximilliancollege.ac.tz

FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA CHUO – SEPTEMBA 2023

1. **Karibu Ndugu** _____

Uongozi wa Chuo St. Maximilliancolbe unayofuraha kuwakaribisha Wanafunzi wote ambao wamechaguliwa kujiunga na chuo chetu pendwa kwa mwaka wa Masomo 2023/2024.

2. **Mahali Chuo Kilipo**

Chuo cha St.Maximilliancolbe kipo Tabora Manispaa, Mtaa wa Ipuli karibu na Shule ya Msingi ya Majengo. Kituo maarufu kilicho karibu na chuo chetu ni Hospitali ya St.Anna.

3. Siku ya kufika chuoni na kuanza Usajili

Wanafunzi wote waliochaguliwa wanatakiwa kufika chuoni kuanzia Tarehe **14-28/08/2023** muda wa saa 2:00 asubuhi hadi saa 12: 00 jioni kwa ajili ya usajili .Muhula wa masomo utaanza kuanzia Tarehe **04/09/2023**.

4. Jumla ya Ada

Jumla ya Ada na michango mingine i.e kitambulisho cha mwanafunzi, chama wa wanafunzi,mafunzo kwa vitendo,mitihani ya ndani,mitihani ya wizara,Ada ya udhibiti ubora ya NACTVET,Hosteli na mahafali

KOZI YA FAMASI

Jumla ya Ada ni **Tsh.** Kwa wanafunzi wa hosteli **2,495,000/=**

Tsh. Kwa wanafunzi wasio wa hosteli **2,095,000/=**

KOZI YA UTABIBU

Jumla ya Ada ni **Tsh.** Kwa wanafunzi wa hosteli **2,725,000/=**

Tsh. Kwa wanafunzi wasio wa hosteli **2,325,000/=**

Social work

Jumla ya Ada ni **Tsh.** Kwa wanafunzi wa hosteli
1,995,000/=

Tsh. Kwa wanafunzi wasio wa hosteli
1,595,000/=

Business Administration

Jumla ya Ada ni **Tsh.** Kwa wanafunzi wa hosteli
1,845,000/=

Tsh. Kwa wanafunzi wasio wa hosteli
1,445,000/=

Malipo mengine ambayo Mwanafunzi anatakiwa alipe kipindi anafanya usajili chuoni ni kama ifuatavyo:

☐**Malipo ya fomu ya usajili yafanyike kipindi cha usajili Tsh. 30,000/=**

☐Rimu ya karatasi **A4 (Kila mwaka) ni sawa na Tsh. 15,000/=**

☐Bima ya AFYA **(NHIF BIMA) Tsh. 50,400/=**

Malipo ya BIMA yatafanyika moja kwa moja kwa NHIF kwa kutumia "Control Number".Malipo mengine yote yalipwe moja kwa moja kwenye akaunti za Benki za Chuo:

*** Kwa Malipo yoyote , Chuo hakipokei Fedha mkononi au malipo kupitia simu za mkononi**

*** Wazazi wanashauriwa kutowapa wanafunzi walipie Ada na michango mingine ya chuo, badala yake walipie moja kwa moja kwenye akaunti za chuo zilizoorodheshwa hapa chini na kuwasilisha risiti kwa Mhasibu wa chuo**

JINA LA AKAUNTI: ST. MAXIMILLIANCOLBE COLLEGE		
1	CRDB BANK	**0150479968300**
2	NMB BANK	**51010016891**

5. **Namna ya kufanya Malipo Kwa wanafunzi wasio wa Hosteli**

Malipo yanaweza kulipwa yote kwa mkupuo au kidogo kidogo kwa awamu 6 kama zilivyoorodheshwa hapa chini ;

KOZI YA FAMASI

JINSI YA KULIPA	**MWEZI**	**MALIPO**
MALIPO YA KWANZA	SEPTEMBER	550,000
MALIPO YA PILI	NOVEMBER	300,000

MALIPO YA TATU	JANUARY	197,500
MALIPO YA NNE	MARCH	550,000
MALIPO YA TANO	MAY	300,000
MALIPO YA SITA	JULY	197,500
JUMLA		**2,095,000**

KOZI YA UTABIBU (CLINICAL MEDICINE)

JINSI YA KULIPA	**MWEZI**	**MALIPO**
MALIPO YA KWANZA	SEPTEMBER	550,000
MALIPO YA PILI	NOVEMBER	350,000
MALIPO YA TATU	JANUARY	262,500
MALIPO YA NNE	MARCH	550,000
MALIPO YA TANO	MAY	350,000
MALIPO YA SITA	JULY	262,500
JUMLA		**2,325,000**

KOZI YA USTAWI WA JAMII (SOCIAL WORK)

JINSI YA KULIPA	**MWEZI**	**MALIPO**
MALIPO YA KWANZA	SEPTEMBER	497,500
MALIPO YA PILI	NOVEMBER	150,000
MALIPO YA TATU	JANUARY	150,000
MALIPO YA NNE	MARCH	497,500
MALIPO YA TANO	MAY	150,000
MALIPO YA SITA	JULY	150,000
JUMLA		**1,595,000**

KOZI YA USIMAMIZI WA BIASHARA (BUSINESS ADMININSTRATION)

JINSI YA KULIPA	**MWEZI**	**MALIPO**
MALIPO YA KWANZA	SEPTEMBER	422,500
MALIPO YA PILI	NOVEMBER	150,000
MALIPO YA TATU	JANUARY	150,000
MALIPO YA NNE	MARCH	422,500
MALIPO YA TANO	MAY	150,000
MALIPO YA SITA	JULY	150,000
JUMLA		**1,445,000**

6. MALIPO YA HOSTELI

Malipo ya Hosteli kwa mwaka Mzima ni Sh. 400,000/= ambayo inalipwa mara mbili (02) kwa Mwaka , kipindi cha Muhula wa kwanza Tsh 200,000/= na Muhula wa pili ni Tsh. 200,000/=

6. Viambatanisho kwa ajili ya usajili

Mwanafunzi anatakiwa aje na vitu vifuatavyo kukamilisha usajili wake:

a. **Nakala ya cheti ya kuhitimu kidato cha nne au nakala ya cheti cha Matokeo(Result Slip)**
b. **Nakala ya cheti cha KuzaliwaCopy of Birth Certificates**
c. **Picha tatu (3) za passpoti zenye rangi ya Bluu kwa nyuma**
d. **Fomu iliyojazwa na Daktari kuonesha hali ya kiafya ya Mwanafunzi**

7. **CHAKULA**

Huduma ya chakula inapatikana chuoni kwa gharama ya Shilingi 3000/= kwa siku (Asubuhi, Mchana na Jioni)

8. SARE

Mwanafunzi atajigharamia sare kwa ajili ya kujiunga na chuo.

➢ WANAFUNZI KOZI YA **FAMASI NA UTABIBU** (CLINICAL MEDICINE)

MWANAFUNZI JINSIA YA KIUME: Suruali mbili za khaki, shati mbili nyeupe zenye mikono mifupi na koti la rangi nyeupe moja.Viatu rangi nyeusi inayofunika miguu na soksi aina mbili (Ni sweta la rangi nyeupe na koti rangi nyeupe tu vinavyoruhusiwa kipindi cha baridi)

MWANAFUNZI JINSIA YA KIKE: Magauni rangi nyeupe marefu mawili, koti moja la rangi nyeupe na koti moja la rangi nyeupe. Viatu rangi nyeusi inayofunika miguu na soksi aina mbili (Ni sweta la rangi nyeupe na koti rangi nyeupe tu vinavyoruhusiwa kipindi cha baridi)

➢ **WANAFUNZI KOZI YA USTAWI WA JAMII (SOCIAL WORK)**

MWANAFUNZI JINSIA YA KIUME: Suruali mbili za rangi ya bluu iliyokolea, mashati mawili ya mikono mirefu, Viatu rangi nyeusi inayofunika miguu na soksi aina mbili (Ni sweta la rangi nyeupe linaruhusiwa kipindi cha baridi)

MWANAFUNZI JINSIA YA KIKE: Sketi ndefu mbili za rangi ya bluu iliyokolea walau urefu wa SM 30 chini ya magoti, Viatu rangi nyeusi inayofunika miguu na soksi aina mbili (Ni sweta la rangi nyeupe linaruhusiwa kipindi cha baridi)

➢ **WANAFUNZI KOZI YA USIMAMIZI WA BIASHARA (BUSINESS ADMINISTRATION)**

MWANAFUNZI JINSIA YA KIUME: Suruali mbili za rangi nyeusi, mashati mawili ya rangi nyeupe, koti moja la suti la rangi nyeusi, Viatu rangi nyeusi inayofunika miguu na soksi aina mbili (Ni sweta la rangi nyeusi linaruhusiwa kipindi cha baridi)

MWANAFUNZI JINSIA YA KIKE: Sketi ndefu mbili za rangi ya bluu iliyokolea walau urefu wa SM 30 chini ya magoti, shati nyeupe mbili za mikono mirefu,koti moja la rangi nyeusi la, Viatu rangi nyeusi inayofunika miguu na soksi aina mbili (Ni sweta la rangi nyeusi linaruhusiwa kipindi cha baridi)